TANGAZO LA SERIKALI NA. 322 la tarehe 26/4/2024

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16 (1))*

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE YA MWAKA 2024

Jina

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe ya Mwaka 2024.

Matumizi

**2**. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe.

Tafsiri

**3**. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo vinginevyo-

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu,

udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"soko" maana yake ni eneo lililotengwa na linalomilikiwa na Halmashauri kwa matumizi ya soko;

"stendi" maana yake ni eneo maalum lililotengwa au kujengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria au mizigo;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii;

Utozaji wa Ada au Ushuru

**4**.-(1) Halmashauri itatoza ada au ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kwa kadiri Halmashauri itakavyoelekeza.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hii zitalipwa kwa Halmashauri.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kulipa ada au ushuru

**5**. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au

*Tangazo La Serikali Na. 322 (Linaendelea)*

ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Muda wa kukusanya ada au ushuru

**6**.-(1) Muda wa kukusanya ada au ushuru utakuwa ni kuanzia Saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi Saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu.

(3) Malipo ya ada au ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yoyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(4) Malipo ya ada au ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

(5) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Mkurugenzi anaweza kutoa kibali maalum kuruhusu shughuli za usafirishaji wa bidhaa yoyote kufanyika nje ya muda ulioainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Ukodishaji wa mali na rasilimali za Halmashauri

**7**.-(1) Halmashauri itapangisha na kukodisha mali na rasilimali zake na kutoza kodi katika majengo, mitambo, nyumba, vibanda vya biashara, viwanja na maeneo ya biashara yanayomilikiwa au kutengwa na Halimashauri katika maeneo yote ya miji na vijiji ndani ya Halmashauri.

(2) Itakua ni wajibu kwa mtu yeyote atakayepanga au kukodi mtambo, nyumba au vibanda au jengo la Halmashauri kuingia mkataba wa upangajii au ukodishwaji wa maandishi kati yake na Halmashauri.

(3) Mtu yeyote atakayeshindwa kulipa kodi ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kupanga au kukodi atafungiwa kibanda au nyumba au kurejesha na kukabidhi

mtambo kwa mmiliki na endapo kibanda au nyumba itaendelea kufungwa kwa sababu hiyo kwa muda wa siku thelathini bila kulipa pango mpangaji huyo atanyang'anywa na atapangishwa mtu mwingine kwa mujibu wa masharti yatakayoainishwa katika mkataba wa upangaji.

(4) Mpangaji hatampangisha mtu mwingine, kuuza au kufanya ukarabati mkubwa wa nyumba au jengo bila idhini ya Halimashauri.

Rejesta katika nyumba za kulala wageni

**8**. Kila mmiliki wa nyumba ya kulala wageni atatakiwa kuandikisha wageni wote katika rejista ya wageni itakayotolewa na Halmashauri baada ya mmiliki wa nyumba ya kulala wageni kulipia ada kwa kiwango kitakachokuwa kimepangwa na Halmashauri.

Wajibu wa kuandaa taarifa.

**9**. Kila mfanyabiashara au mtoa huduma katika Halmashauri atakuwa na wajibu wa kuandaa na kutunza taarifa za biashara au huduma yake.

Utoaji wa stakabadhi za malipo

**10**.-(1) Ada au ushuru utakaotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, utalipwa kwa Halmashauri au kwa Wakala ambaye atatoa stakabadhi ya kielektroniki kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

(2) Utakuwa ni wajibu wa kila mlipa ada au ushuru kudai na kuhakiki stakabadhi ya malipo kulingana na kiasi cha fedha alicholipa.

(3) Utakuwa sio utetezi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, mtu kudai kuwa amelipa ada au ushuru lakini hakupewa stakabadhi ya kielektroniki.

Ukusanyaji wa madeni

**11**.-(1) Halmashauri inaweza kukusanya ushuru kwa njia ya mahakama endapo mtu halisi, kikundi, taasisi au kampuni itakuwa imeshindwa kulipa ada au ushuru kwa muda uliokubaliwa.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), Halmashauri

inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali zinazohamishika za mdaiwa zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Baada ya kipindi cha siku thelathini kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuziuza kabla hazijaharibika baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(5) Bila kuathiri ya kanuni ndogo ya (3) na (4), Halmashauri kabla ya kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma juu ya kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote ile itakayotokea ama wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri au Wakala.

Uteuzi wa Wakala

**12.**-(1) Halmashauri itakuwa na Mamlaka ya kuteua Wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, kukusanya ada au ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea ada au ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii; na

(b) kukusanya ada au ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

*Tangazo La Serikali Na. 322 (Linaendelea)*

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

**13**. Bila kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Makosa

**14**.-(1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:

(a) atashindwa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;
(c) atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kulipiwa ada au ushuru;
(e) atashindwa kuweka kumbukumbu, vitabu, hesabu, au maelezo yoyote yatakayohitajika na Halmashauri;
(f) atashindwa, atadharau, atakaidi au kukataa kulipa ada au ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii;
(g) atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha kutengeneza au atatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri; au
(h) atatumia chombo chochote cha usafiri kusafirishia bidhaa ambayo haijalipiwa ushuru

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA • THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

au ada.

Adhabu

**15**. Mtu atakayetiwa hatiani kwa kukiuka masharti ya Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua Shilingi laki mbili na kisichozidi Shilingi Milioni moja au kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka miwili au vyote.

Kufililisha kosa

**16**. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha Shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa TS. Na. 482 la, 2015

**17**. Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe ya Mwaka 2015 inafutwa.

---

**JEDWALI LA KWANZA**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(1))*

ADA NA USHURU WA VIBALI, LESENI NA HUDUMA MBALIMBALI

SEHEMU YA KWANZA

Ushuru wa Minara na Matangazo/Mabango

| Namba | Aina ya Huduma | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Maombi ya kufanya matangazo ya biashara au promosheni Kwa siku kwa kutumia vipaza sauti | 50,000/= kwa siku |
| 2. | Matangazo mengineyo yahusuyo masuala ya kijamii kwa kutumia vipaza sauti | 5,000/= kwa siku |
| 3. | Picha Jongefu. | 50,000/= kwa siku |

*Tangazo La Serikali Na. 322 (Linaendelea)*

SEHEMU YA PILI
Ada za kukodisha Mali za Halmashauri

| Namba | Aina ya kifaa | Kiwango cha Ada au Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Banda la Mgahawa | 40,000 kwa mwezi |
| 2. | Kisadeko ya zamani | 50,000 kwa mwezi |
| 3. | Kisadeko mpya | 200,000/= kwa mwezi |
| 4. | Sehemu ya kuoshea vyombo vya moto (car wash) | 40,000/= kwa mwezi |
| 5. | Gereji ya vyombo vya moto | 40,000/= kwa mwezi |
| 6. | Choo cha umma kituo kipya | 100,000 kwa mwezi |
| 7. | Choo cha umma kituo cha zamani | 50,000 kwa mwezi |
| 8. | Kutumia choo cha umma cha kulipia | 300 |
| 9. | Nyumba ya chumba kimoja | 30,000 kwa mwezi |
| 10. | Nyumba ya vyumba viwili | 50,000 kwa mwezi |
| 11. | Nyumba ya vyumba vitatu | 70,000 kwa mwezi |
| 12. | Jengo la ofisi | 100,000 kwa mwezi |
| 13. | Banda la biashara kituo cha zamani cha mabasi | 40,000 kwa mwezi |
| 14. | Banda la biashara kituo kipya cha mabasi | 80,000 kwa mwezi |
| 15. | Banda la biashara uwanja wa mpira bombani | 20,000 kwa mwezi |
| 16. | Banda la biashara la Halmashauri | 40,000 kwa mwezi |
| 17. | Trekta | 50,000 kwa siku |
| 18. | Lori | 10,000 kwa siku |
| 19. | Ukumbi kwa ajili ya mikutano au vikao | 100,000 kwa masaa 8 |
| 20. | Ukumbi kwa ajili ya sherehe | 200,000 kwa masaa 8 |
| 21. | Machine ya kushindilia | 30,000 kwa siku |
| 22. | Maegesho ya kulaza gari katika gereji | 1,000 kwa siku |
| 23. | Uwanja wa mpira | 100,000 kwa Ligi |
| 24. | Kukodisha mitambo mingine | 50,000 kwa siku |

*Tangazo La Serikali Na. 322 (Linaendelea)*

## SEHEMU YA TATU

Ada ya Mabaraza ya Kata

| Namba | Huduma | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Kufungua shauri | 5,000/= |
| 2. | Kuhamisha Baraza | 40,000/= |
| 3. | Upekuzi wa Jalada | 5,000/= |

## SEHEMU YA NNE

Ushuru wa Usafirishaji Mazao ya mbao

| Jina la kinachosafirishwa | Kiwango/Idadi | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| Mlango wa mbao mpya | 1 | 10,000/= |
| Dirisha la mbao jipya | 1 | 10,000/= |
| Kitanda cha mbao kipya | 1 | 20,000/= |
| Meza/Kiti cha mbao kipya | 1 | 10,000/= |
| Mipini | 1 | 300/= |
| Miko/Chanuo/Vinu/Mikeka/Vigoda/Vikapu | 1 | 300/= |
| Magome/Mizizi/Majani/Vijiti | Kilo1 | 1,000/= |
| Kindu/Matete/Mianzi | M3 1 | 1,000/= |

## SEHEMU YA TANO

Ada za Vibali

| Namba | Aina ya Kibali | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| A | Vibali vya Ujenzi | Ada |
| 1. | Kiwanja cha makazi pekee | 500/=kwa mita za mraba |
| | Kiwanja cha huduma za jamii | 300/= kwa mita za mraba |
| | Kiwanja cha Makazi na Biashara | 600/= kwa mita za mraba |
| | Kiwanja cha biashara na viwanda | 700/= kwa mita za mraba |
| 2. | Ukaguzi wa ramani za nyumba kwa ajili ya kibali cha ujenzi | 30,000/= |
| B | Vibali vya Shughuli mbalimbali | |

*Tangazo La Serikali Na. 322 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Sherehe | |
| | Mshereheshaji na Music | 20,000/= kwa siku |
| | MC | 20,000/= kwa siku |
| | Mpiga picha | 20,000/= kwa siku |
| | Mpambaji | 20,000/= kwa siku |
| | Chakula | 20,000/= kwa siku |
| | Vinjwaji | 20,000/= kwa siku |
| 2. | Ngoma | 10,000/= kwa siku |
| 9. | Muziki | 20,000/= kwa siku |
| 10. | Mikutano ya adhara isipokuwa ya dini na siasa | 10,000/= kwa siku |
| 11. | Kongamano | 20,000/= kwa siku |
| 12. | Uhamasishaji | 20,000/= kwa uhamasishaji |
| 13. | Tamasha | 500,000/= kwa siku |
| 14. | Bonanza | 100,000/= kwa shindano |
| 15. | Ushoroba Festival | 500,000 kwa siku |
| 16. | Mashindano ya michezo | 100,000/ kwa shindano |
| 17. | utafiti | 50,000/= kwa tafiti |
| 18. | Shughuli zingine ambazo hazijatajwa | 30,000/= kwa siku |
| 19. | Holding fee | 30,000/= kwa mwaka |

SEHEMU YA SITA

Ada za Huduma za Mifugo

| Namba. | MFUGO | MNADA | MACHINJIO | USAFIRISHAJI | CHANJO/DAWA | UKAGUZI | ULINZI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 4,000 | 1,500 | 4,000 | 1,000 – 10,000 | 1,500 | 20,000 kwa Siku kwa Mlinzi |
| 2. | Mbuzi | 1,500 | 600 | 1,500 | 500 – 5,000 | 600 | |
| 3. | Kondoo | 1,500 | 600 | 1,500 | 500 – 5,000 | 600 | |
| 4. | Nguruwe | 1,500 | 600 | 1,500 | 500 – 5,000 | 600 | |
| 5. | Sungura | 500 | 500 | 500 | 500 – 5,000 | 500 | |
| 6. | Mbwa | 1,000 | - | 1,500 | 500 – 5,000 | Uteketezaji | 100,000 |
| 7. | Paka | 500 | - | 500 | 500 – 5,000 | Uteketezaji | 100,000 |
| 8. | kuku | 200 | - | - | 200 – 5,000 | 500 | - |

*Tangazo La Serikali Na. 322 (Linaendelea)*

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 9. | Bata | 200 | - | - | 200 – 5,000 | 500 | - |
| 10. | Kanga | 200 | - | - | 200 – 5,000 | 500 | - |
| 11. | Njiwa | 200 | - | - | 200 – 5,000 | 500 | - |
| 12. | Mingine | 200 – 4000 | 0 - 1500 | 0 – 1000 | 200 – 5,000 | 500 | - |

SEHEMU YA SABA

Ushuru wa Madini

| Namba | Aina ya Madini | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mawe | 6,000 kwa tani |
| 2. | Mchanga | 2,000 kwa tani |
| 3. | Kifusi | 1,500 kwa tani |
| 4. | Kokoto | 6,000 kwa tani |
| 5. | Kaolin (dongojasi) | 3,000 kwa tani |
| 6. | Chokaa | 2,000 kwa tani |
| 7. | Fidia ya utunzaji mazingira kwa viwanda na machimbo | 1,500,000 kwa mwaka |

SEHEMU YA NANE

Ushuru wa Ukusanyaji wa Takangumu

| Namba | Aina ya Biashara au Huduma | kiwango cha ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Makazi (Kaya) | |
| (a) | Kundi lenye kipato cha juu | 10,000 kwa mwezi |
| (b) | Kundi lenye kipato cha kati | 5,000 kwa mwezi |
| (c) | Kundi lenye kipato cha chini | 2,000 kwa mwezi |
| 2. | Mgahawa mkubwa | 15,000 kwa mwezi |
| 3. | Mgahawa mdogo | 10,000 kwa mwezi |
| 4. | Nyumba ya kulala wageni | 20,000 kwa mwezi |
| 5. | Zahanati (taka zisizo hatari) | 15,000 kwa mwezi |
| 6. | Kituo cha afya (taka zisizo hatari) | 20,000 kwa mwezi |
| 7. | Hospitali (binafsi) | 50,000 kwa mwezi |
| 8. | Kiwanda cha kuuza mbao | 20,000 kwa mwezi |
| 9. | Fundi seremala wakubwa | 10,000 kwa mwezi |
| 10. | Fundi seremala wadogo | 3,000 kwa mwezi |

*Tangazo La Serikali Na. 322 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 11. | Fundi chuma | 15,000 kwa mwezi |
| 12. | Karakana | 20,000 kwa mwezi |
| 13. | Kiwanda kidogo | 20,000 kwa mwezi |
| 14. | Kiwanda kikubwa | 100,000 kwa mwezi |
| 15. | Duka la jumla | 20,000 kwa mwezi |
| 16. | Duka la rejereja/huduma vijijini | 5,000 kwa mwezi |
| | Duka la rejareja/huduma mji mdogo | 10,000 kwa mwezi |
| 17. | Shule ya Msingi ya Bweni (binafsi) | 20,000 kwa mwezi |
| 18. | Shule ya msingi ya kutwa (binafsi) | 10,000 kwa mwezi |
| 19. | Shule ya Sekondari ya kutwa (binafsi) | 15,000 kwa mwezi |
| 20. | Shule ya Sekondari ya Bweni (binafsi) | 30,000 kwa mwezi |
| 21. | Duka dogo la chakula | 10,000 kwa mwezi |
| 22. | Duka kubwa la chakula | 30,000 kwa mwezi |
| 23. | Baa | 20,000 kwa mwezi |
| 24. | Klabu ya usiku | 20,000 kwa mwezi |
| 25. | Kumbi za Sherehe | 20,000 kwa mwezi |
| 26. | Duka la kuuza nyama na samaki | 10,000 kwa mwezi |
| 27. | Duka la dawa (Jumla na Rejareja) | 10,000 kwa mwezi |
| 28. | Duka la dawa (Rejareja) | 10,000 kwa mwezi |
| 29. | Dobi mkubwa | 20,000 kwa mwezi |
| 30. | Fundi wa vifaa vya umeme | 5,000 kwa mwezi |
| 31. | Fundi kushona | 3,000 kwa mwezi |
| 32. | Saluni | 10,000 kwa mwezi |
| 33. | Kituo cha kuuza mafuta | 30,000 kwa mwezi |
| 34. | Stoo | 5,000 kwa mwezi |
| 35. | Ghala | 10,000 kwa mwezi |
| 36. | Hoteli: | |
| | (a) ya kitalii | 30,000 kwa mwezi |
| | (b) ya kawaida | 15,000 kwa mwezi |
| 37. | Taasisi | 50,000 kwa mwezi |
| 38. | klabu ya pombe ya asili | 5,000 kwa mwezi |
| 39. | Kituo cha michezo | 5,000 kwa mwezi |
| 40. | Uwanja wa michezo | 20,000 kwa mwezi |
| 41. | Washona viatu | 2,000 kwa mwezi |
| 42. | Stoo za mkaa | 10,000 kwa mwezi |
| 43. | Mama Lishe na Baba Lishe | 5,000 kwa mwezi |
| 44. | Vituo vya kuoshea magari | 50,000 kwa mwezi |
| 45. | Aina nyingine ya biashara/huduma | Ada itapangwa na kamati ya kudumu husika na chanzo hicho kila itakapo |

*Tangazo La Serikali Na. 322 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| | | hitajika kwa mwezi |
| 46. | Ubomoaji na uondoaji mabaki ya vifaa vya ujenzi kwa mita moja ya mraba | 5,000 kwa kazi |

SEHEMU YA TISA

Ushuru wa kulaza vyombo vya usafiri maeneo yanayomilikiwa na Halmashauri

| Namba | Aina ya Chombo cha Usafiri | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Basi kubwa | 2,000/= kwa siku |
| 2. | Basi dogo | 1,000/= kwa siku |
| 3. | Gari ndogo (pick up) | 1,000/= kwa siku |
| 4. | Lori lenye uwezo wa kubeba tani 2 hadi 5 | 2,000/= kwa siku |
| 5. | Lori lenye uwezo wa kubeba tani 6 hadi 10 | 5,000/= kwa siku |
| 6. | Kuingia kituo cha mabasi lenye uwezo wa kubeba abiria 30 na zaidi | 2,000 kwa safari |
| 7. | Kuingia kituo cha mabasi lenye uwezo wa kubeba abiria 15 hadi 29 | 1,000 kwa safari |
| 8. | Kuingia kituo cha mabasi lenye uwezo wa kubeba abiria 1 hadi 14 | 500 kwa safari |
| 9. | Kuingia kituo cha mabasi kwa teksi, pikipiki na bajaji. | 1,000 kwa safari |
| 10. | Kuingia kituo cha mabasi kwa kwa magari yasiyo ya abiria. | 1,000 kwa safari |

SEHEMU YA KUMI

Gharama za utupaji taka kwenye jalala la taka

| Namba | Kiasi cha taka | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Chini ya tani moja | 50,000/= kwa safari |
| 2. | Tani moja | 40,000/= kwa safari |

*Tangazo La Serikali Na. 322 (Linaendelea)*

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA

### Ushuru wa Mazao ya Misitu

| Namba | Aina ya Mazao | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Aina zote za mazao ya Misitu. | Asilimia tano (5%) ya Mrabaha wa Serikali Kuu |
| 2. | Mbao (Mijengo, mikurunge na milunda) | 500/=kwa kila ubao |
| 3. | Mche wa matunda na isiyo ya matunda | 100/=kwa kila mche |
| 4. | Mkaa gunia au kiloba kilo 50 | 3,000/=kwa kila gunia |
| 5. | Mkaa gunia au kiloba cha kati chini ya kilo 50 | 2,000/=kwa kila gunia |
| 6. | Mkaa gunia au kiloba cha kati chini ya kilo 50 | 1,000 |
| 7. | Kuni kwa mita za mraba | 3,000/= kwa mita za mraba |
| 8. | Ushuru wa mazao ya kilimo kwa mnunuzi Asilimia 3 ya bei ya Mauzo | |
| 9. | Ushuru wamauzo ya kiwanja/shamba/eneo lisilopimwa asilimia kumi (10%) ya mauzo | |
| 10. | Bei ya tofali ni asilimia 25 ya gharama za uzalishaji kujumlisha gharama za uzalishaji na itakuwa ikikokotolewa na kutangazwa na Mkurugenzi Mtendaji Wilaya. | |
| 11. | Bei ya korosho ni asilimia 25 ya gharama za uzalishaji kujumlisha gharama za uzalishaji na itakuwa ikikokotolewa na kutangazwa na Mkurugenzi Mtendaji Wilaya. | |
| 12. | Bei ya bidhaa au malighafi zitakazo zalishwa na Halmashauri ni asilimia 25 ya gharama za uzalishaji kujumlisha gharama za uzalishaji na itakuwa ikikokotolewa na kutangazwa na Mkurugenzi Mtendaji Wilaya. | |

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI

### Ada ya Utalii

| Namba | Huduma/Eneo | Mgeni wa nje | Mgeni wa nje mtoto umri miaka 7-16 | Mgeni wa nje mkazi | Mgeni wa nje mkazi motto umri miaka 7-16 | Watanzania | Watanzania watoto umri wa miaka7-16 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Boma la Kisangire | 20,000 | 10,000 | 10,000 | 5,000 | 3,000 | 1,000 |

*Tangazo La Serikali Na. 322 (Linaendelea)*

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2. | Vimondo | 10,000 | 5,000 | 5,000 | 2,500 | 2,000 | 1,000 |
| 3. | Panga la Mwingereza | 10,000 | 5,000 | 5,000 | 2,500 | 2,000 | 1,000 |
| 4. | Chuo cha Biblia Maneromango | 20,000 | 10,000 | 10,000 | 5,000 | 3,000 | 1,000 |
| 5. | Majengo ya Minaki | 20,000 | 10,000 | 10,000 | 5,000 | 3,000 | 1,000 |
| 6. | Ada ya Kambi kwa siku | 20,000 | 10,000 | 10,000 | 7,000 | 6,000 | 2,000 |
| 7. | Utafiti katika maeneo ya malikale | Asilimia tano ya bajeti ya Utafiti. | | | | | |

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

*Tangazo La Serikali Na. 322 (Linaendelea)*

**JEDWALI LA PILI**

*(Limetengenezwa Chini ya aya ya 16)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFILILISHA KOSA

Mimi ........................................................................nakiri KWA HIARI YANGU MIMI MWENYEWE mbele ya.......................................................... ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe kwamba Tarehe ..........ya Mwezi .................. Mwaka................ nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya Kifungu cha …….. cha Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe ya Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe, Niko tayari kulipa kiasi cha ada au ushuru na faini ninayodaiwa.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo Tarehe ......................ya Mwezi ................................Mwaka ……
Jina: ..................................................
Saini: .................................................
MBELE YA:
Jina……..............................................
Wadhifa: ............................................
Saini: .................................................
Tarehe: ...............................................

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA · THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA · PROFESSIONALISM & EXCELLENCE

*Tangazo La Serikali Na. 322 (Linaendelea)*

Nembo ya Halmashauri ya wilaya ya kisarawe imebandikwa katika Sheria Ndogo hizi kufutia maamuzi ya yaliyopitishwa na kikao cha Halmashauri kilichofanyika tarehe 10 mwezi Mei 2023 Muhuri huo umepigwa mbele ya:-

BETRICE R. DOMINIC
*Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe*

ZUBERI J. KIZWEZWE
*Mwenyekiti wa Halmashauri*
*Halmashauri ya Wilaya Kisarawe*

NAKUBALI

L.S

Dodoma,
25 March, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi- Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*